

Simu:+255 684 291 102  
Barua pepe: dedbuchosa@gmail.com  
www.buchosadc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Buchosa  
44 Buchosa,SENGEREMA

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza John Mongela, leo tarehe 05 Mei 2017 ameshiliki katika zoezi la ufyekaji na uteketezaji wa bangi katika Hifadhi ya msitu wa Buhindi katika kijiji cha Ilyamchele kata ya Kazunzu Wilayani Sengerema.

Katika uteketezaji huo Mkuu wa Wilaya ya Sengerema Emmanuel Kipole amemueleza mkuu wa Mkoa wa Mwanza John Mongela kuwa Wilaya ya Sengerema imejipanga katika maeneo manne katika kutokomeza matumizi ya bangi pamoja na madawa mengine ya kulevya.

**“Mheshimiwa mkuu wa Mkoa tumejipanga kutokomeza kadhia hii katika maeneo manne, maeneo hayo ni uzalisha, usafirishaji, uzaji na utumiaji”** amesema Kipole.

Uteketezaji huo wa Bangi umehusisaha watumishi wa ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa, watumishi wa Hifadhi ya msitu Buhindi pamoja na vikosi mbalimbali vya Ulinzi na Usalama vya Mkoa wa mwanza.

Akizungumza baada ya uteketezaji wa Bangi Mkuu wa mkoa John Mongela amemuagiza mkuu wa Wilaya ya Sengerema Emmanuel Kipole kuhakikisha mifugo yote iliyomo kwenye hifadhi hiyo inatolewa na kutoruhusu shughuli za kibinadamu ndani ya msitu huo kufanyika.

Pia mkuu wa Mkoa John Mongela amewashukuru raia wema wanaoendelea kutoa taarifa za uhalifu na kuwezesha kuzuia kwa matendo ya uovu katika maeneo yao.

**“niwapongeze sana wananchi watoa taarifa”** amesema Mongela.

Zoezi la uteketezaji na ufyekaji bangi limefanyika sanjari na agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. John Pombe Magufuli ikiwa ni mapambano dhidi ya kutokomeza madawa ya kulevya nchi nzima.

Edward A. Mwasakafyuka  
Kaimu Afisa Habari, Halmashauri ya Wilaya Buchosa  
SENGEREMA